# Shaaban Robert na Utetezi wa Mwanamke: Mfano wa Siti Binti Saad

**Kitula King'ei**


## Ikisiri

*Shaaban Robert ni mwasisi na mlezi wa fasihi andishi ya Kiswahili. Kati ya machapisho yake muhimu yanahusu ushairi, riwaya, insha na hadithi fupi.*

*Wahakiki wengi wa fasihi ya Kiswahili (k.m. Kezilahabi 1976; na Wafula 1989) wamezingatia sana maudhui yake ya kisiasa, maadili, utu na ucha Mungu pamoja na matumizi yake ya lugha ya kitamathali kama vile taswira-jazanda, methali na mafumbo. Hata hivyo, miongoni mwa kazi za Shaaban Robert zinazosifika ni hadithi ya kiwasifu iitwayo, 'Wasifu wa Siti Binti Saad', (1967), ni kazi yenye maudhui mazito na yanayooana na masuala ibuka katika jamii ya leo. Haya ni maswali yanayohusu nafasi ya mwanamke katika jamii na haja ya mwanamke kujitosa katika ulimwengu wa ushindani wa kijinsia ili kudhihirisha na kuendeleza vipawa vyake. Haya ndiyo yanayoshughulikiwa katika makala haya. Mhakiki anachunguza mawazo, misimamo na imani za Shaaban Robert kuhusu mwanamke kama kiumbe dhidi ya mwanamume. Anachunguza mbinu na maarifa ya mtunzi wa wasifu huu na jinsi anavyomwasilisha mhusika wake mkuu; namna Siti anavyoonyesha kujiamini na ujasiri katika kuyashinda matatizo na vikwazo vya kifamilia, kijamii, kijinsia na hata kiuchumi na kuibuka mshindi.*

*Funzo kuu hapa ni kuwa Shaaban Robert alitimiza lengo lake kuu ambalo lilikuwa kuthibitisha mwanamke hatakiwi kubakia katika unyonge na udhaifu wa jinsia na mazingira yake bali anapaswa kuwa na ukakamavu wa kushindania hadhi, heshima na nafasi yake ya kujikimu na kuikimu familia yake. Kwa kushindana vilivyo na wanaume na taasubi zao za kijadi, mwanamke atawaweza kujishindia utukufu na heshima yake kama alivyoonyesha Siti Binti Saad.*


## 1.0 Utangulizi

Shaaban Robert ni kati ya waasisi wa taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Katika umri wake (1909 hadi 1962), alijitahidi sana kuchangia maendeleo na kuenea kwa sanaa hii licha ya magumu mengi yaliyomkabili. Kwanza, kabisa, mazingira ya utawala wa kikoloni yalifanya kazi ya mwandishi yeyote wa Kiafrika kuwa ngumu sana na nafasi za uchapishaji zilikuwa finyu mno. Mara kwa mara, Shaaban Robert alijibidiisha kupeleka miswada yake Afrika Kusini ili ipigwe chapa. Isitoshe, hata baada ya kupata bahati ya kuchapishiwa miswada yake, mwandishi huyu hakulipwa mrabaha kwa mauzo ya kazi hizo ingawa aliteta mara kwa mara na wachapishaji hao kuhusu jambo hili (Achebe, 1975).

Kutokana na mapenzi yake makuu ya kutunga na kuandika kazi za fasihi, Shaaban Robert alijinyima mengi ili kutayarisha kazi hizo. Kwanza, mwandishi huyu alikuwa na kiwango kidogo cha elimu lakini alijaliwa wingi wa maarifa, hekima na moyo wa ujasiri. Kipawa chake cha utunzi hakina kifani hapa Afrika Mashariki, hasa katika utunzi wa tungo zenye undani wa kimantiki. Isitoshe, Shaaban Robert alikuwa mfanyakazi wa umma na alifanya kazi kwa muda mrefu kama mtumishi wa serikali mwenye cheo cha Karani Mkuu na hata kupandishwa

ngazi kazini mara kadhaa kutokana na bidii na uaminifu wake. Licha ya kubanwa kiwakati kutokana na ajira yake, Shaaban Robert hakukosa wasaa wa kutulia na kututungia kazi za kifasihi zenye kusisimua na kuelimisha.

Miongoni mwa machapisho yake Shaaban Robert ambayo vizazi baada ya vizazi vimefaidi ni:

*Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*
*Kusadikika*
*Kufikirika*
*Wasifu wa Siti Binti Saad*
*Masomo Yenye Adili*
*Insha na Mashairi*
*Kielelezo cha Fasili*
*Sanaa ya Ushairi*
*Utubora Mkulima*
*Siku ya Watenzi Wote*
*Mashairi ya Shaaban Robert*
*Mwafrika Aimba*
*Almasi za Afrika*
*Ashiki Kitabu Hiki*
*Mapenzi Bora*
*Pambo la Lugha*
*Adili na Nduguze*

Tungo hizi za Shaaban Robert zilijumuisha tanzu nyingi za kifasihi na mwandishi alijipambanua na kujidhihirisha kama msanii wa kipekee. Tunaweza kusema kuwa mtunzi alifikia kiwango cha juu cha usanifu katika kila aina ya utanzu aliouandikia, yaani, ushairi, hadithi (angalia k.m. *Adili na Nduguze* aliyoibuni upya na kuitafsiri kutoka Mkusanyiko wa *Arabian Nights* (Bertoncini, 2009). riwaya na hata insha. Hadithi zake nyingine zinazosifika sana, ambazo huitwa vijiriwaya au riwaya ni pamoja na *Kusadikika, Kufikirika* na *Utubora Mkulima*. Hadithi hizi zimesheheni maudhui kuhusu uongozi wa kidemokrasia, kupinga itikadi zisizofaa na ushirikina pamoja kushadidia uadilifu na utu katika tabia ya mwanadamu, mtawalia.

Mbali na maudhui yaliyotajwa hapo juu, Shaaban Robert pia amewahi kujishughulisha na kutetea hadhi, utu na heshima ya mwanamke siyo tu katika ushairi wake bali pia katika kazi zake za kinathari. Maudhui haya ya kumkomboa mwanamke kutokana na minyororo ya kimaumbile, familia na siasa, yamepewa nafasi kubwa sana katika maandishi ya Shaaban Robert. Wahakiki wengi wa kazi za mwandishi huyu wanaafikiana kuwa, kwa ujumla, kuna ushahidi unaothibitisha fika kwamba, "Kimsingi, hakuna hata riwaya moja ya Shaaban Robert iliyoacha kumthamini mwanamke..." (Chuachua 2011: 140). Kwa mfano, katika kuendeleza maudhui ya ukombozi wa mwanamke, kitabu chake Robert kiitwacho,

*Wasifu wa Siti Binti Saad* ni cha kipekee miongoni mwa machapisho ya tungo za mwandishi huyu mahiri. Sababu ya kwanza ya kudai hivi ni kuwa hii ndiyo kazi yake ya pekee ambayo ameitunga kwa kufuata kitanzu au kipera cha "wasifu." Pili, tawasifu hii ni ya kipekee ya mwandishi huyu inayosimulia maisha ya mhusika mkuu akiwa ni mwanamke. Mpaka leo, karibu miaka hamsini sasa tangu kuchapishwa kwa *Wasifu wa Siti Binti Saad* katika mwaka wa 1967, kazi za wasifu ni chache mno katika fasihi ya Kiswahili.

Makala haya mafupi yanadhamiria kuchanganua mawazo ya Shaaban Robert kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii. Hoja kuu hapa ni kwamba Shaaban Robert alitumia siyo tu riwaya hii ya wasifu bali pia ushairi wake ili kupigania hadhi ya mwanamke. Kimsingi hii ni sifa muhimu sana ya utunzi wake, kwani sote tunatambua kuwa katika jamii na enzi alizoishi Robert, kiumbe wa kike hakupewa nafasi aliyostahili hasa kutokana na amali za kitamaduni zilizovyaza mitazamo hasi dhidi yake. Kwa mfano, wasichana wengi nyakati hizo walinyimwa nafasi ya kujipatia elimu na hivyo kukosa ajira ya maana ya kujikimu maishani. Bila kuchelea pingamizi au hata shutuma kutoka kwa wanajamii hawa waliozingatia sana falsafa ya kimapokezi kuwa mwanamke ni kiumbe duni asiyeweza kushindana na mwanamume katika jambo lolote na kwamba mahala pake mwafaka ni nyumbani kuzaa, kulea, na kuwatunza wanawe pamoja na mumewe; Shaaban Robert alijitolea kuhadithia maisha ya mwanamke; shujaa na mwenye haiba na ukakamavu ambaye pia hakuogopa kujitokeza kunoa kipawa chake na kushindana na wanaume.

### 1.1 Misingi ya Kinadharia

Kuna mitazamo kadha ya uhakiki wenye misingi ya utetezi wa haki za wanawake katika taaluma nyingi za kijamii kama vile fasihi, lugha, sosholojia, historia, siasa na hata uchumi. Mifano ya nadharia kama hizi ni zile za awali sana za Kimagharibi kama vile Marekani na Uropa ambazo zinajumuisha wahakiki kama Woolf (1929), Wollstonecraft (1792), Beauvoir (1952) ambao wanachunguza itikadi za kijadi zinazomnyima mwanamke haki zake za kibinadamu. Asasi wanazoangazia ni pamoja na ndoa, uzazi, malezi, dini na utamaduni kwa jumla.

Tapo la pili la wananadharia wa utetezi wa mwanamke ni lile lenye kuangazia wahusika na usawiri wao katika fasihi na pia matumizi yao ya lugha ambalo mwakilishi wake anayetambulika sana ni Mary Eagleton (1991). Katika *Wasifu wa Siti Binti Saad* na pia baadhi ya mashairi yake, Shaaban Robert alizingatia sana falsafa ya kumtetea mwanamke. Hata hivyo, yeye alijiepusha na mitazamo mikali ya wanaharakati kama ule wa "Wafeministi" au ule wa kuangalia masuala ya ugandamizwaji wa mwanamke kwa macho ya kike pekee kama wafanyavyo wananadharia wa mtazamo-kike wanaojulikana kwa Kiingereza kama *gynaocritics*. Badala yake, Shaaban Robert anatilia mkazo ukosoaji wa mila,

amali, itikadi na mielekeo hasi dhidi ya mwanamke. Jukumu lake ni kuonyesha umuhimu wa kumkomboa mwanamke kutokana na utamaduni mzima wenye kumfunga silisili za kumzuia kujiendeleza akiwa mwenzi wa mwanamume. Yeye kamwe hawalaumu wanaume kwa masaibu ya wanawake bali anatambua kuwa utamaduni unaomdunisha mwanamke ndio adui wa mwanamke.

## 1.2 Falsafa ya Mwandishi kuhusu Mwanamke

Tungo nyingi katika fasihi ya Kiswahili zimekuwa zikiwasawiri wahusika wa kike kwa njia hasi kuanzia tendi au tenzi za zamani kama vile, *Utendi wa Mwanakupona* uliotungwa mnamo mwaka 1858 (Wamitila, 2002). Hata hivyo, ni dhahiri kuwa baadhi ya kazi chache katika fasihi huwaonesha wahusika wa kike kwa njia chanya. Mfano mzuri ni huu wa riwaya ya Shaaban Robert, *Wasifu wa Siti Binti Saad.* Isitoshe, sehemu kubwa ya mashairi yake Shaaban Robert yanadhihirisha mzinduko na mwamko mkubwa kuhusu umuhimu wa kumpa mwanamke heshima na hadhi anayostahiki kama mwanadamu. Kwa mujibu wa Kezilahabi (1976: 54-55), Shaaban Robert aliwastahi sana wanawake katika kazi zake zote.

Mfano mzuri ni huu hapa:

*UA*

*E ua la manukato, katika maisha yangu*
*Na faraja ya uzito, kila aina machungu*
*Kwangu ua hili shoto, na kulia pia yangu*
*Na lifumuapo woto, ni pambo la ulimwengu*
*Ua hili kama kito, ua hili kufu yangu.*

*Ni ua kweli si ndoto, ua ni kipenzi changu*
*Ni ua lenye mnato, limevuta moyo wangu*
*Tokea mimi moto, ni lenye mapenzi yangu*
*Ua li kando ya mto, neema kubwa ya Mungu*
*Ua lina zari fito, zenye kiwiti cha mbingu.*

*Ua limejirembato, kadiri ya pambo langu*
*Ua hunizima joto, machungu ya ulimwengu*
*Kisha likawasha mto na bidii kubwa kwangu*
*Nalo hapewi mtoto, tampa mpenzi wangu*
*Ua halina majuto, halidhiki walimwengu.*

*Ua lanipa manyeto, majivuno kwa wenzangu*
*Nendako sina kisito, narudi nyumbani kwangu*
*Nyuki hukosa mng'ato, kwa ladha ua langu*
*Na asali yake nzito, huwa ni kinywaji changu*

*Ua hili ni kioto, makao ya ndege wangu.*

*Ndege nimempa poto, ya johari za mizungu*
*Ili asipate koto, nami nashukuru Mungu,*
*Kwamba hafanyi fukuto, ananiridhi kwa yangu*
*Aniridhi kwa mazito, na makali na machungu*
*Ua lenye kipeto, nawekea siri yangu.*

Kwa kutumia jazanda kama "ua" na "johari" pamoja na taswira nyingine, mshairi anamsawiri mwanamke kuwa kiumbe wa thamani kuu na pia anabainisha wazi kwamba uhusiano wa mwanamke na mwanamume hukamilika na kufana tu katika asasi na mazingira ya ndoa. Waswahili husema, 'mwanamke ni anga la nyumba' na hapa mshairi anatukumbusha hilo kwa kutusimulia jinsi mke mzuri anavyompa mumewe fahari, furaha, amani na hata imani. Kumfananisha mwanamke na kitu cha kupendeza kama ua siyo kumdunisha wala kumwonyesha kuwa ni kitu cha kumvutia na kumpumbaza tu mwanamke. Hili si kweli hata kidogo. Lengo la mwandishi ni kuonyesha mwanamke ni mwenzi wa mwanamume na kwamba wote wawili wanakamilishana. Upendo kati yao ndio msingi wa utu wao.

Maudhui kama hayo ya kumstahi na kumtukuza mwanamke yanapatikana katika shairi "Mke Mwema" kutoka katika diwani ya Shaaban Robert iitwayo, *Insha na Mashairi.*

*MKE MWEMA*

*Cheo cha mtu hupanda, ukipata mke mwema,*
*Kula chachu na maganda, mfano kama mnyama,*
*Na nyumba iwe kibanda, si nzuri ya kutazama,*
*Utaona umewanda, moyo umekuterema.*

*Mke mwema ni johari, yenye furaha daima,*
*Awe hasa na saburi, na adili na huruma,*
*Hata ukiwa fakiri, hutimizi pato jema,*
*Utajiona tajiri, maliki dunia nzima.*

*Mke akiwa mbishi, wa kushindana kusema,*
*Na majivuno na mashi, na ulimi wake pima,*
*Hata kama wala pishi, wali na kilo ya nyama,*
*Utajiona waishi, dunia huna kima.*

*Mke mrembo si hoja, hili nimekwisha pima,*
*Nimepima rejareja, kila jambo kutazama,*
*Kujumlisha pamoja, mambo yalivyosimama,*
*Nikaona kuwa tija ndogo kuliko gharama.*

*Awe mwema mke wangu, nani hapendi kusema?*
*Wema asili ya ungu, milele una heshima,*
*Kuwa wema walimwengu, ni wajibu na lazima,*
*Wema dawa ya machungu moyoni yanayouma.*
(S. Robert, *Insha na Mashairi*, uk. 22-23)

Ni dhahiri hapa kuwa mshairi anasisitiza umuhimu wa kumpata mke mwema na faida anazozipata mume kwa kuwa na mke kama huyo. Mwishoni anashauri kuwa kila mwanadamu awe mke au mume, anawajibika kuwa mwema kimaadili kwani, wema unatoka kwa Mungu, Muumba wa vyote. Kauli hii ni ushahidi kuwa Shaaban Robert hakuwabagua watu kwa misingi ya jinsia zao bali aliwahesabu kuwa ni wanadamu waliolingana na kukamilishana kwa kila hali.

### 1.4 Hoja zaUtetezi wa Mwanamke katika Wasifu wa *Siti Binti Saad*

Kwanza anatanguliza wasifu huu wa maisha ya mwanamke aitwaye Siti Binti Saad kwa kumsifia kwa kipawa chake cha usanii wa kimuziki ambacho kilimfanya apendwe katika eneo zima la Afrika Mashariki. Katika ubeti mfupi amemsifia hivi:

*Alikuwa ni kinanda*
*Afrika Mashariki*
*Na watu wakampenda*
*Kwa hawa na kwa ashiki*
*Ndipo bidii ikenda*
*Kutunga kitabu hiki.*
*(WWSBS, uk. x)*

Shaaban Robert ameshaeleza katika tungo mbili tulizopitia hapo juu kwamba uzuri au urembo wa mwanamke si hoja alimradi tu awe na wema na tabia njema. Katika riwaya yake hii, *Wasifu wa Siti Binti Saad* (kuanzia sasa WWSBS) anasimulia mwanzo kuwa ingawa Siti hakujaliwa sura ya kuvutia, aliposwa na kuolewa bila tatizo kwani alikuwa mwenye kupendwa akapendeka.

*Hata kama Siti hakuwa na sudusu ya uzuri wa Zuhura, lakini hilo halikuwa pingamizi ya furaha ya arusi kumjia. Kama wanawake wengine, aliposwa kwa shauku na mapenzi mengi sana akaolewa na Rajabu, mume aliyekuwa kufu yake.*
*(WWSBS, uk. 5)*

Kwa nini Siti aliolewa licha ya kuwa na sura isiyopendeza? Shaaban Robert alijibu swali hili kwa kusema:

> *Sura maalum ilikuwa si kinywaji cha kuzima kiu kali ya mapenzi. Mapenzi yalitii zaidi amri ya shauku kuliko yalivyotii ushawishi wa sura (WWSBS, uk. 6).*

Siti ameonyeshwa kuwa kiumbe mwenye sifa za ajabu kwani alikuwa na subira, unyenyekevu na imani kuu iliyomwezesha kuyashinda majaribu na mitihani aliyokumbana nayo. Kama walivyotufunza wahenga, "Atangaye kwa jua hujua" na kuwa "Mchumia juani hulia kivulini." Siti alifanikiwa licha ya vikwazo vingi. Tunaelezwa kuwa:

> *Aliishi maisha ya kukumbukwa milele juu ya pingamizi zake za ujinga wa kusoma, umaskini na unyonge. Hili lilikuwa jambo kubwa sana kwa mwanamke wa cheo chake. Alionyesha johari iliyoweza kupatikana kwa mwanamke kama mila iliyomnyima ushirika iliwezekana kushindiwa (WWSBS, uk.13).*

Tunazidi kufahamishwa kuwa siyo tu kuwa Siti aliyashinda mashaka na vikwazo vilivyomwandama, bali alitimiza hilo kwa njia ya haki na ya kiungwana. Kwa hivyo, Siti alidhihirisha kiwango cha juu cha uadilifu. Ndipo mwandishi akasisitiza:

> *Siti alikuwa si mmoja wa wahuni waliozoea kutoroka kwao wakakimbilia katika miji kukaa kama chaza juu ya mwamba au kama kupe na mkia wa ng'ombe (WWSBS, uk. 13).*

Isitoshe, miongoni mwa matatizo aliyoyashinda Siti ni ile aibu ya kusimangwa kuwa ana sauti nzuri lakini sura mbaya na hali yake pia ilikuwa duni mno kwani hata alitembea bila viatu huku akiwa kavaa matambara tu. Pili na muhimu zaidi, ni kushinda hali ya woga wa kuimba mbele ya hadhira mara ya kwanza. Watu wengi wangekumbana na jambo kama hilo, wangeambaa sanaa ya uimbaji milele daima lakini Siti aliyavumilia na akaendelea kujaribu. Hizi ni sifa ambazo ni nadra sana kupatikana miongoni mwa watu wenye mioyo midogo na waliojaa hofu ya kujaribu jambo na kuendelea kujaribu hata baada ya kukosa kufaulu mara ya kwanza au hata ya pili.

Kwa ufupi, mwandishi anasema kuwa Siti alijitahidi kuyakimu maisha yake kwa haki na kwa uungwana bila kumtia yeyote mrija au kujivunjia heshima yake. Alinuia kupata ufanisi siyo kwa kutegemea kutiliwa upodo au kupendelewa na

yeyote bali hasa kwa ustahiki wake mwenyewe. Hizi ni sifa nyingine muhimu za mwanamke huyu, Siti Binti Saad.

Siti amepewa sifa nyingine zinazostahili kuigwa na wanawake wengine hata katika jamii yetu ya sasa. Sifa mojawapo ni kuwa mwenye bidii ya nyuki au ya mchwa. Shaaban Robert anasema:

> *Utamu wa mazao ya jasho lake ulipozidi naye alizidi, naye alizidi kufanya kazi kwa bidii vilevile. Mwendo wake ulikuwa kama huu siku zote. Alihudhuria katika taarabu kadha wa kadha katika mji wa Unguja akaimba mchana na usiku kama kurumbizi (WWSBS, uk. 16).*

Siti pia ameoneshwa kuwa mwanamke mwadilifu na mcha Mungu. Hii ni sifa ya kimsingi kwa vile utu wake wote umebainisha uungwana, upole, heshima na nia njema kutokana na imani hii yake ya kidini. Mtunzi ametueleza:

> *Siti alikuwa mwanamke mcha Mungu wa sala na saumu.*
> *Alisali vipindi vitano kila siku, akafunga faradhi na saumu*
> *katika masiha yake yote (WWSBS, uk. 17).*

Hata hivyo, mwandishi anamchora Siti siyo kama kiumbe ambaye ana sifa ya malaika lakini hasa mwenye sifa ya binadamu wa kawaida aliyeshiriki ibada na pia mambo ya kidunia. Hata hivyo, alifanya hivyo kwa busara na hekima wala maisha yake hayakuwa na ukinzani wowote kati ya maslahi yake ya ibada na mahitaji yake ya kilimwengu. Kwa maneno yake, mwandishi anasema kuwa:

> *Siti alikuwa mtu wa ibada katika wakati wa ibada.*
> *Alikuwa mtu wa malimwengu kama wengine*
> *wakati wa ada za ulimwengu (WWSBS, uk. 18).*

Licha ya ufanisi mkubwa aliofikia, Siti alibakia mnyenyekevu na mpole wala hakuonesha kiburi au majisifu. Tunafahamishwa kuwa:

> *...mwanamke huyu hakuharibika kwa fanaka, fedha na*
> *wafanyakazi waliolipwa mishahara kila mwezi katika*
> *nyumba zake (WWSBS, uk. 20).*

Pale maadui na mahasidi wake Siti walipomkashifu kuwa alikuwa maskini, mshamba na kama siyo Mungu kumjalia kipawa cha sauti nzuri ya kuimba angeangamia, mwandishi anamtetea kwa kusema kuwa wale waivu na adui zake Siti walikuwa watu ambao walikosa utu na ustaarabu. Robert anamsifu na kumtetea Siti siyo tu kwa kuwa jasiri na mkakamavu hata akaweza kujiingiza katika uwanja wa mashindano makali dhidi ya wanaume, bali hasa kwa kutekeleza

hayo yote kwa unyenyekevu mwingi licha ya uchokozi wa maadui zake. Kwa kuchukua hatua hii licha ya hali yake duni na sura iliyokosa mvuto, Siti alionyesha mfano mzuri na kuwa kielelezo katika maendeleo ya wanawake katika Afrika Mashariki. Mahasidi wake Siti walimtusi na kumdunisha kwa kumwimba hivi:

*Siti Binti Saad;*
*Umekuwa mtu lini?*
*Ulitoka shamba,*
*Na kaniki mbili chini,*
*Kama si sauti;*
*Ungekula nini? (WWSBS, uk. 22)*

Katika jibu lake dhidi ya matusi ya madui zake kwamba alikuwa duni na maskini, mwandishi alimfanya Siti kuwa mnyenyekevu na pia mwenye busara kuu. Kutokana na jibu lake, Siti aliwadhihirishia wapinzani wake kuwa wapumbavu na wafidhuli kwa kumrushia matusi bila sababu zozote. Alisisitiza kuwa upungufu mkubwa wa mwanadamu siyo kuwa na sura isiyopendeza lakini kupungukiwa na akili. Jibu lake Siti lilikuwa hivi:

*Si hoja uzuri*
*Na sura jamali,*
*Kuwa mtukufu*
*Na jadi kubeli,*
*Hasara ya mtu*
*Kukosa akili (WWSBS, uk. 29).*

Jibu hili la kiungwana liliwaacha madui zake Siti vinywa wazi wasijue la kusema tena kwani hawakumtegemea Siti kuwajibu kwa upole kama huo. Pengine wao walitarajia angewajibu vibaya kwa matusi kama yale waliyokuwa wamemrushia. Kweli ya aushi katika jawabu la Siti ilikuwa kwamba, kila mwanadamu anayemdharau mwenzake huwa anabainisha ujinga na utovu wa busara.

Baada ya kushambuliwa na madui zake kuwa mwenye sura mbaya na maskini hohehahe, Siti pia alishutumiwa kuwa kwa kujiingiza katika ushindani dhidi ya wanaume na kwa kuacha maisha yake ya shamba na kuishi mjini, ati alikuwa ameivunja familia yake na kuasi mila pia. Watesi wake walishikilia imani na itikadi ya jadi kwamba mahali pa mwanamke ni nyumbani na jukumu lake la kipekee ni kulea wanawe na kumtunza mumewe. Wao hawakutambua kuwa mwanamke ana uhuru wa kuchagua mahali pa kuishi na kazi ya kufanya. Kwa mara nyingine tena, Siti aliwajibu watesi wake kwa kusisitiza kuwa hakuwa

amekusudia kuvunja jamii bali alifuata tu majaliwa yake, kwani, wahenga walinena kuwa, "Liandikwalo ndilo liwalo." na "bidii ya mja haiondoi kudura" Kwa ufupi, Siti aliwajibu kama ifuatavyo:

*Si kusudi langu,*
*Kuvunja watani,*
*Enyi walimwengu,*
*Mwajua yakini,*
*Apendalo Mungu,*
*Haliwezekani (WWSBS, uk. 30).*

Siti alizidi kudhihirisha falsafa yake ya busara, uwekevu na mantiki ya uadilifu. Alijipambanua kama mwalimu wa jamii ambaye hakusita kuielekeza na kuifundisha sifa za utu wa kweli katika mashairi ya nyimbo zake. Katika mfano ufuatao, Siti anatufundisha tuwe na busara ya kutosemasema ovyo au kutobubujikwa na maneno bali tuwe wenye kutahadhari. Kusema mambo ya kibinafsi hadharani ni sawa na kujiumbua. Kuna maneno yafaayo kusemwa na kuna yale yanayostahili kuhifadhiwa sirini. Ndipo wazee wakatufunza kuwa, "Penye kuku wengi, usimwage mtama". Wimbo tunaorejelea hapa ni huu:

*Siri sifunue*
*Kwa wino wa rangi,*
*Fahamu ujuwe*
*Kuna mambo mengi,*
*Wajila mwenyewe*
*Kwa ujinga mwingi (WWSBS, uk. 42).*

Kama asemavyo mtunzi Shaaban Robert, Siti hapa alijidhihirisha kuwa mwenge wa kumulika johari katika pembe za giza za moyo wa mwanadamu.

**Hitimisho**

Kwa nini Shaaban Robert aliamua kuandika wasifu wa Siti Binti Saad na kumrundikia sifa sufufu kutokana na utu na kazi yake ya uimbaji? Kuna sababu kadha, alizotoa mwandishi. Kwanza kabisa, Siti alikuwa mwenye kipawa cha sauti ambacho alikitumia vyema na kupata ufanisi mkubwa kama mwanasanaa aliyesifika kote Afrika Mashariki. Alitembelea nchi kadha kwa mwialiko maalumu ikiwamo nchi za Bara Hindi. Pili, Siti alistahili sifa kwa kuwa mwanamke wa kwanza Afrika Mashariki kujitokeza kushindana na wanaume katika sanaa ya uimbaji na biashara ya muziki. Tatu, Siti alituachia mfano mwema au kielelezo cha kuigwa na wasichana ama wanawake wa janibu na enzi hizi. Kwa mfano, kutokana na kazi yake tunajifunza kwamba si hoja wala si sababu ya kushindwa ikiwa mtu ametoka katika jamii duni, tabaka lisilofahamika, hali ya

uchochole au kukosa elimu rasmi. Yote haya ni changamoto zinazoweza na zinazofaa kushindwa. Utu wa mtu hautegemei mambo kama haya. Haya yote ni vizingiti au vikwazo ambavyo mhusika atavishinda iwapo ana imani, mwelekeo, nia njema, uadilifu, bidii, ujasiri, nidhamu na moyo wa kujitolea. Kama anavyotuasa mwandishi Shaaban Robert:

> *Mtu yeyote aliyeweza kutenda tendo bora alikuwa bora, potelea mbali wazazi wake walikuwa kina nani, kabila gani au rangi gani ( WWSBS, uk. 50).*

Katika miaka 30 ya uimbaji wake, Siti alitunga na kuimba zaidi ya nyimbo elfu nne za taarabu (King'ala, 1987). Huu ni mchango mkubwa katika ukuzaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili. Kutokana na kipawa chake cha utunzi na uimbaji, Siti Binti Saad ameingia katika vitabu vya kumbukumbu katika sanaa ya Kiswahili. Sote hatuna budi kumstahi Shaaban Robert kwa kututungia wasifu wa Siti ambaye, bila shaka siyo tu gwiji wa uimbaji na utunzi wa nyimbo, bali pia mfano mwema wa uongozi na ufanisi katika sanaa. Kwa kweli, mutribu mwenzake Siti aliyeitwa Mwalimu Shaaban, hakukosea alipomtungia Siti wimbo maalumu wa kutambua umaarufu wake. Aliimba maneno ambayo yanasheheni fikra nzito na yanatupa muhtasari wa maisha ya Siti pale aliposema:

> *Siti wa sitara*
> *Na umaarufu,*
> *Na wingi wa haya*
> *Na ujamilifu,*
> *Pokea hedaya*
> *Ingawa dhaifu ( WWSBS, uk. 32).*

## Marejeleo


Beauvoir, Simone de ( 1952). *The Second Sex.* New York: Modern Library.

Bertoncini, E. na wenzie (2009). *Outline of Swahili Literature.* Leiden: Brill.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert.* Dar es Salaam: TUKI.

Eagleton, M. (1991). *Feminist Literary Criticism.* London: Longman.

Kezilahabi, E. (1976). *Ushairi wa Shaaban.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

King'ala, Y. (1987). *Mwongo wa Wasifu wa Siti Binti Saad* Nairobi: East African Publishing House.

Robert, S. (1967). *Insha na Mashairi*. Nairobi: Nelson.
Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix.
Wafula, R. (1989). "The Use of Allegory in Shaaban Robert's Proseworks". (Haijachapishwa) Tasinifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
Woolf V.( 1929). *A Room of One's Own and Three Guineas*. New York: Harcourt.
Wollstonecraft, M. (1792). *A Vindication of the Rights of Woman*. Boston: Peter Edes.